Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-272-510-510

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**EMMANUEL YUSUF @ NORIEGA**

**DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**SHAURI NA. 013/2018**

**HUKUMU KUHUSU USTAHIKI NA FIDIA**

**26 JUNI 2025**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, tarehe 26 Juni 2025**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) leo imetoa hukumu katika kesi ya *Emmanuel Yusuf @ Noriega dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Emmanuel Yusuf @ Noriega (Mleta Shauri), ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Shauri). Alidai kufanyika ukiukaji wa Vifungu vya 3(1), 3(2), 5 na 7 vya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba).

Mjibu Shauri aliibua pingamizi dhidi ya mamlaka halisi ya Mahakama kulingana na ukweli kwamba mahakama za ndani zilikuwa zimetoa uamuzi kuhusu masuala yaliyoibuliwa na Mleta Shauri. Mahakama ilithibitisha kwamba ingawa si chombo cha rufaa, ina mamlaka ya kuangalia endapo kesi zinazoendesha katika mahakama za ndani zinazingatia viwango vya haki za binadamu. Iliamua kuwa ilikuwa na mamlaka ya kisheria kwa kuwa Mleta Shauri alidai kufanyika ukiukaji wa Kifungu cha 3, 5, na 7 cha Mkataba ambao Mjibu Shauri ni mhusika. Kwa hivyo, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi la Mjibu Shauri kuhusu *mamlaka yake ya kisheria.*

*Kuhusu* vipengele vingine vya mamlaka, Mahakama ilibaini kwamba ilikuwa na mamlaka binafsi kwani Shauri hilo liliwasilishwa kabla ondoleo la Azimio la Mjibu Shauri chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki) halijaanza kutumika. Pia iliona kuwa ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulikuwa wa hali ya kuendelea, na kwenye mamlaka ya kieneo kwani ukiukaji huo ulitokea ndani ya eneo la Mjibu Shauri. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Shauri hilo.

Kuhusu ukubalifu, Mjibu Shauri hakutoa pingamizi lolote lakini alitoa wito kwa Mahakama kutangaza kwamba Shauri hili halikubaliki. Mahakama iliona kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Itifaki, kilichorejelewa katika Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Mahakama (Kanuni), lazima iamue ukubalifu wa kesi zilizowasilishwa mbele yake. Kwa hivyo, Mahakama iliendelea kuangalia endapo Shauri hili lilikidhi matakwa yote ya ukubalifu yaliyoainishwa katika Kifungu cha 56 cha Mkataba na kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 50 ya Kanuni za Mahakama.

Mahakama ilibaini kwamba, kulingana na kumbukumbu, matakwa ya ukubalifu yaliyowekwa chini ya Kanuni za 50(2)(a), 50(2)(b), 50(2)(c), na 50(2)(d) za Kanuni za Mahakama yalitimizwa. Kuhusu matakwa ya kukamilisha taratibu za ndani kwa mujibu wa Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama, Mahakama ilibainisha kwamba matakwa ya kukamilisha taratibu za ndani yalikuwa yametimizwa kwa kuwa Mahakama ya Rufaa, chombo cha juu cha mahakama cha Mjibu Shauri, ilikuwa imeshughulikia kesi hiyo na kutupilia mbali rufaa yote ya Mleta Shauri tarehe 27 Oktoba 2009.

Kuhusiana na matakwa yaliyo chini ya Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama, kwamba Mashauri lazima yawasilishwe ndani ya muda unaofaa baada ya kukamilisha taratibu zote za ndani, Mahakama ilirejelea uamuzi wake kwamba tathmini ya matakwa hayo ni kulingana na kesi moja moja. Mahakama iliona kwamba katika Shauri hili hatua ya kuanza kuhesabu muda ilikuwa tarehe 29 Machi 2010,

ambapo Mjibu Shauri aliwasilisha Azimio lake, kwa kuwa hatua hii iliruhusu watu binafsi kuwasilisha madai dhidi yake. Pia ilibaini kuwa kipindi cha kati ya mwaka 2007 na 2013 kilikuwa ni miaka ya kuundwa kwake na kwamba wakati wa kipindi hiki, umma kwa ujumla, achilia mbali watu walio katika hali ya Mleta Shauri hawakuweza kudhaniwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uwepo wa Mahakama.

Mahakama ilizingatia mazingira ya Mleta Shauri, ikiwa ni pamoja na kufungwa kwake jela akisubiri kifo, hali ambayo ilimzuia kupata habari na msaada wa kisheria. Kwa kuzingatia sababu hizi zisizozuilika, Mahakama ilibaini kwamba kipindi cha miaka mitano kilikuwa kinafaa kwa mujibu wa Kifungu cha 56(6) cha Mkataba kikisomwa pamoja na Kanuni ya 50(2)(f).

Hatimaye, Mahakama ilidhibiti kwamba Shauri hili halikuhusu kesi ambayo tayari imetatuliwa na Wahusika kwa mujibu wa kanuni za Mkataba wa Umoja wa Mataifa, Sheria ya Katiba ya Umoja wa Afrika, au masharti ya Mkataba, hivyo kutimiza Kanuni ya 50(2)(g).

Kwa hivyo, kwa kuangalia mazingatio haya yote, Mahakama iliamua kwamba Shauri hili lilikidhi matakwa yote ya ukubalifu na ikatangaza kuwa yanakubalika.

Kuhusu uzingatiaji wa sheria, Mahakama ilibaini kwamba Mleta Shauri alishindwa kuthibitisha madai yake ya ukiukaji wa haki za usawa na ulinzi sawa wa sheria, kuhusiana na jinsi mahakama za ndani zilivyoendesha kesi yake. Kwa hivyo Mahakama iliona kwamba Mjibu Shauri hakukiuka Kifungu cha 3(1) na (2) cha Mkataba katika suala hili.

Aidha, iliona kwamba hakukuwa na ukiukaji wa haki ya Mleta Shauri ya kusikilizwa kwa haki kuhusu wasaidizi wa mahakama kushindwa kuwahoji mashahidi, kama ilivyohakikishwa chini ya Kifungu cha 7(1) cha Mkataba.

Hata hivyo, Mahakama ilibaini kuwa Mjibu Shauri alikiuka haki ya utu ya Mleta Shauri na haki ya ulinzi dhidi ya adhabu ya kikatili, ya kinyama, au ya kudhalilisha chini ya Kifungu cha 5 cha Mkataba. Ukiukaji huu ulitokana na kushindwa kwa Jaji wa Amani,

akifanya kazi kama wakala wa Mjibu Shauri, kuagiza uchunguzi wa haraka ufanyike kuhusu madai ya ukatili wa polisi dhidi ya Mleta Shauri. Mahakama ilisisitiza umuhimu wa kuhakikisha kwamba madai yote ya unyanyasaji, hasa yale yanayofanywa kizuizini, yanachunguzwa kwa kina na kwa haraka.

Kuhusu madai ya ukiukaji wa haki ya kujitetea, Mahakama ilirejelea busara yake ya kisheria kwamba mshtakiwa anayekabiliwa na mashtaka makubwa ya jinai lazima apewe msaada wa kisheria bila malipo endapo hana njia za kupata uwakilishi, na pale ambapo maslahi ya haki yanahitaji ifanyike hivyo, bila ulazima wa kuomba. Mahakama ilibaini kwamba, kutokana na uzito wa kesi ya Mleta Shauri na ugumu wa uendeshaji wa kesi za kisheria, alipaswa kupewa msaada wa kisheria wenye ufanisi, na kushindwa kufanya hivyo ni ukiukaji wa Kifungu cha 7(1)(c) cha Mkataba kama kinavyosomwa pamoja na Kifungu cha 14(3)(d) cha ICCPR. Mahakama iliamua, kwa uamuzi wa wengi wa majaji saba waliounga mkono na watatu waliopinga, kwamba Mjibu Shauri pia alikiuka haki ya Mleta Shauri ya kusikilizwa kwa haki kwa kushindwa kumhukumu ndani ya muda unaofaa, kama inavyotakiwa chini ya Kifungu cha 7(1)(d) cha Mkataba.

Ingawa madai haya hayakutoka kwa Mleta Shauri, Mahakama, *kwa hiari yake*, pia iliona kwamba Mjibu Shauri alikiuka haki ya kuishi ya Mleta Shauri, kama inavyolindwa chini ya Kifungu cha 4 cha Mkataba, kwa kutoa adhabu ya kifo kwa njia ya lazima bila kuruhusu maafisa wa mahakama kuwa na busara ya kuzingatia asili ya kosa na hali binafsi ya mshtakiwa. Uamuzi huu uliafikiwa na wengi kwa idadi ya majaji wanane, na waliopinga wawili. Aidha, Mahakama ilibaini kuwa kutolewa kwa adhabu ya kifo kwa kunyongwa ni ukiukaji wa haki ya utu ya Mleta Shauri na haki ya kutopewa adhabu ya kikatili, ya kinyama, au ya kudhalilisha chini ya Kifungu cha 5 cha Mkataba.

Kuhusu fidia, Mahakama, kulingana na busara zake za kisheria, ilitupilia mbali maombi ya Mleta Shauri kuhusu fidia kuhusiana na hasara ya mali ikizingatiwa kwamba madai hayo hayakuthibitishwa.

Kuhusu hasara ya kimaadili, Mahakama ilibainisha kwamba haki za Mleta Shauri kuhusiana na kusikilizwa kwa haki, haki ya kuishi, na utu zilikiukwa, hali ambayo ilisababisha mateso makubwa ya kisaikolojia na kimwili, ikiwa ni pamoja na kuzorota kwa hali ya afya na msongo wa mawazo kutokana na kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu na kwa kupewa adhabu ya kifo. Kwa kuzingatia uzito wa ukiukaji huu, Mahakama ilimpa Mleta Shauri Shilingi za Tanzania Milioni Moja (TZS 1,000,000) kama fidia ya hasara ya kimaadili. Hata hivyo, Mahakama ilitupilia mbali maombi ya fidia kwa waathiriwa wasio wa moja kwa moja, kwani Mleta Shauri hakutoa ushahidi wa kutosha kuhusu utegemezi wao au hasara waliyopata.

Kuhusu fidia isiyo ya kifedha, Mahakama ilitupilia mbali maombi ya Mleta Shauri kwamba aachiliwe huru ikizingatiwa kwamba ukiukaji uliobainika haukuathiri hukumu na hatia. Kinyume chake, Mahakama iliamuru Mjibu Shauri achukue hatua zote muhimu za kubatilisha adhabu ya kifo aliyohukumiwa Mleta Shauri na amwondoe kwenye gereza la wafungwa wanaosubiri kunyongwa. Mahakama pia iliamuru Mjibu Shauri arekebishe sheria zake na kuondoa adhabu ya kifo ya lazima na kunyongwa kama njia ya kutekeleza hukumu ya kifo. Mahakama iliamuru kwamba hukumu hiyo ichapishwe ndani ya miezi mitatu na kumwamuru Mjibu Shauri aripoti kuhusu utekelezaji wa maagizo hayo kila baada ya miezi sita hadi yatakapotekelezwa kikamilifu.

Hatimaye Mahakama iliamuru kila Mhusika abebe gharama zake mwenyewe.

**<u>Kwa maelezo zaidi</u>:**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na maelezo yote ya Hukumu ya Mahakama ya Afrika yanapatikana kwenye tovuti: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0132018

Kwa maswali mengine yote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni Mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi za Afrika ili kulinda Haki za Binadamu na Watu barani Afrika. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org*